Tangazo la Serikali Namba 448 la Tarehe 7 Novemba 2014

SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA WILAYA)

(SURA YA 287)

SHERIA NDOGO.

Zimetungwa chini ya Kifungu cha 153.

SHERIA NDOGO ZA (USAFI WA MAZINGIRA) HALMASHAURI YA WILAYA YA LUDEWA, 2014.

Jina na tarehe ya kuanza kutumika.

1. Sheria ndogo hizi zitajulikana kama Sheria ndogo za (Usafi wa Mazingira) za Halmashauri ya Wilaya Ludewa, 2014 na zitaanza kutumika baada ya kuchapishwa katika Gazeti la Serikali.

Eneo la kutumika.

2. Sheria ndogo hizi zitatumika katika eneo lote lililopo chini ya Mamlaka ya Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa.

Tafsiri ya maneno.

3. Katika Sheria ndogo hizi isipokuwa pale itakapoelezwa vinginevyo:-

"Afisa Afya" maana yake ni Afisa yeyote wa Afya aliyeajiriwa na Halmashauri.

'Afisa Muidhiniwa' maana yake ni Afisa yeyote wa Halmashauri aliyeteuliwa kusimamia utekelezaji wa Sheria ndogo hizi.

"Chakula" maana yake ni kitu chochote kinacholiwa au kunywewa na binadamu isipokuwa madawa hii ni pamoja na:-

a) Kitu chochote kinachotumika katika matengenezo ya chakula;
b) Kitu chochote kinachoongeza ladha ya chakula;
c) Kitu chochote kinachobadili rangi ya chakula (binzari n.k)

'Choo' maana yake ni chumba maalum ambacho kimejengwa kwa ajili ya kuhifadhi kinyesi cha binadamu.

"eneo la wazi" maana yake ni eneo lililochini ya mamlaka ya Halmashauri ambalo limekatazwa kufanyia shughuli ambayo haihusiani na matumizi yaliyokusudiwa.

'Halmashauri' maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa.

"kero" maana yake ni kitu chochote ambacho kipo katika hali yoyote au kinatumika au kimewekwa, kimejengwa au ni kichafu kiasi cha kusababisha:-

a) Hatari kwa viumbe au maisha ya mwanadamu;
b) Harafu mbaya na kuudhi;
c) Magonjwa kwa binadamu, hifadhi ya mbu, inzi, panya na viumbe wengine waletao madhara.

"Majani" maana yake ni majani yote marefu, vichaka vyenye urefu wa sentimeta 15 au zaidi vinavyopatikana sehemu yoyote ndani ya Halmashauri, hii ni pamoja na mazao marefu yanayolimwa maeneo yaliyokatazwa.

Sheria Na.20 ya mwaka 2004.

"Maji taka" kama ilivyoelezwa katika Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ni pamoja na taka zinazotokana na kinyesi, mkojo, uchafu wa majimaji kutoka majumbani, taasisi,ya mjengo ya biashara na viwandani.

"Mabomba ya maji machafu" maana yake ni mabomba yanayotumika kuchukua maji machafu kutoka majumbani au kwenye mifereji ya maji machafu au ya mvua ni pamoja na bomba lolote lililowazi kupitisha maji machafu au ya mvua.

"Mkazi" maana yake ni raia wa Tanzania ambaye kwa kawaida anaishi kwenye eneo lililoko chini ya Mamlaka ya Halmashauri na ambaye ama ana kaya au anaishi katika kaya au taasisi iliyopo katika eneo la Halmashauri.

‘Mkurugenzi’ maana yake ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa pamoja na Afisa yeyote wa Halmashauri atakayeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi.

‘Nyumba za vyakula” maana yake ni hoteli, mgahawa, magenge ya vyakula na inajumuisha mahali popote panapouzwa vyakula vyovyote vilivyopikwa na visivyopikwa.

“Wanyama” maana yake Ng’ombe, Mbwa, Kondoo, Punda, Nguruwe ikiwa na mnyama yeyote anayefugwa na binadamu.

“Shimo” ina maana eneo lolote lililochimbwa kwa kazi kuhifadhi takataka.

Sheria Na.20 ya mwaka 2004

“taka” kama ilivyoelezwa katika Sheria ya Usimamizi wa Mazingira maana yake ni kitu chochote kimiminika, kigumu, gesi na mionzi, kinachotoa harufu mbaya au kilichohifadhiwa katika mazingira ya hali ya ujazo, uozo au hali nyingine yoyote inayosababisha uharibifu wa mazingira ambayo inajumuisha taka.

“Usafi wa mazingira” maana yake ni usafi wa mazingira yanayozunguka binadamu kuwa katika hali isiyoweza kuleta madhara kwake na wengine, hii ni pamoja na maji, miti, hewa, ardhi na wanyama pamoja na viumbe visivyo hai kama vile nyumba.

Wajibu wa kufanya usafi na kutunza mazingira.

4(1) Mtu yeyote ambaye anaishi, kufanya biashara au shughuli yoyote kwenye nyumba ya kuishi, biashara au taasisi yoyote iliyoko eneo la Halmashauri anawajibika.

a) Kuweka mazingira yanayomzunguka katika hali ya usafi muda wote kwa kuharibu mazalia ya mbu.
b) Anajenga choo imara chenye upana wa futi 4 kwa 4 kilichojengwa kwa matofali na kuezekwa kwa bati au nyasi na kinachotumika muda wote.
c) Takataka au uchafu wowote unakusanywa na kufukiwa au kuondolewa kwa njia itakayoelekezwa na Halmashauri;
d) Anachimba shimo la kutupia takataka litakalokuwa na upana usiopungua futi 2 kwa futi 2 au pipa la kuhifadhi takataka;
e) Anafanya matengenezo ya nyumba yake mara kwa mara kila inapoharibika;
f) Eneo lake la kufanyia biashara lina kuwa katika hali ya usafi na kwa maduka ya chakula na dawa yanakuwa yamesajiliwa na Mamlaka ya Chakula na Dawa (TFDA)

(2) Itakuwa ni kosa kwa mtu yeyote kumwaga takataka za aina yoyote katika mtaa au mahali popote ambapo hakuna shimo au pipa bila idhini ya Halmashauri.

(3) Itakuwa marufuku kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi kulima mazao yenye urefu zaidi ya sentimeta 15 katika maeneo yote yaliyozuiliwa na Halmashauri.

Ujenzi wa nyumba bora na choo.

5. Itakuwa ni lazima kwa kila mkazi wa Halmashauri anayejenga nyumba ya kuishi kuimarisha jengo wakati wa kujenga kwa kutumia tofali na kuezeka kwa bati au nyasi. Nyumba inapaswa iwe na madirisha ya kutosha pamoja na choo kama ilivyoelezwa katika Sheria Ndogo hizi.

Uwezo wa Afisa Mwidhiniwa

6(1) Afisa Mwidhiniwa atakuwa na uwezo wa kuingia katika jengo lolote ndani ya mamlaka ya Halmashauri na kufanya ukaguzi kama kuna kero yoyote na kumataka mtu anayehusika na kero hiyo kuiondoa katika muda atakaopewa na Afisa Mwidhiniwa.

(2) Kutakuwa na ada ya uzoaji taka na ukaguzi wa mazingira ya biashara kwa viwango vilivyooneshwa kwenye majedwali ya sheria ndogo hizi ambayo italipwa kwa Halmashauri au wakala atakayeteuliwa na Halmashauri kwa kazi hiyo.

Wajibu wa wahudumu kupima afya

7. Itakuwa ni wajibu wa kila mhudumu wa hoteli, mgahawa, baa, nyumba za kulala wageni, bucha, waoka mikate, bisi au mtu yeyote anayeshughulika na kuuza vyakula vilivyopikwa kuhakikisha kwamba anapimwa afya yake mara moja kila baada ya miezi mitatu pamoja na kuwa na kibali cha Halmashauri kinachomruhusu kuendesha biashara hiyo atakacholipia shilingi elfu moja kila baada ya miezi mitatu.

Maji taka

8 Itakuwa ni marufuku kwa mtu yeyote kuacha shimo la maji machafu wazi au kumwaga maji au taka, kutapisha ama kuruhusu kumwaga au kutapisha au kuruhusu kufurika choo, karo, septic tank, soakage pit, cepool au kuruhusu kupasuka au kuziba bomba la maji taka kutoka ndani ya nyumba na kuyatiririsha kwenye barabara, njia, kichaka, eneo la burudani ama sehemu nyingine isiyokusudiwa.

Wajibu wa kutoa taarifa za magonjwa au vifo

9(1) Itakuwa ni wajibu wa kila mtu atakayekuwa na habari au mashaka ya mtu au mnyama yeyote wa kufugwa na binadamu kuugua ugonjwa usio wa kawaida au ugonjwa wa kuambukiza kwa njia ya hewa kutoa taarifa kwa Mkurugenzi au Mganga Mkuu au Afisa Mwidhiniwa.

(2) Baada ya kupokea taarifa za ugonjwa Mkurugenzi au Mganga Mkuu anaweza kutoa amri ya kuondoa watu wote katika nyumba ambayo ugonjwa huo umetokea, au kunyunyizia dawa za kuulia viini vya ugonjwa, au kupulizia dawa au kuharibu vitu endapo itaonekana kwamba vitu hivyo vina viini vya magonjwa.

(3) Endapo itathibitika kuzuka kwa ugonjwa wa mlipuko Mkurugenzi atamtaarifu Mkuu wa Wilaya juu ya kuzuka kwa ugonjwa huo na Mkuu wa Wilaya anaweza kutoa amri ya maandishi juu ya namna ya kuzuia na kudhibiti ugonjwa huo usienee.

Kupiga kelele

10. Itakuwa ni marufuku kwa mtu yeyote kufungulia muziki kwa sauti ya juu ambayo itasababisha makelele na kuwa kero kwa wakazi wengine.

Upikaji na uuzaji wa chakula

11(1) Halmashauri itakuwa na uwezo wa kuzuia upishi na uuzaji wa vyakula katika mazingira yasiyoridhisha kiafya.

(2) Itakuwa ni marufuku kwa mtu yeyote kutengeneza au kuuza chakula mtaani, uchochoroni, magengeni au kwenye nyumba yoyote mpaka awe ametimiza masharti na kanuni za afya na awe amepata kibali kutoka Halmashauri.

Mazingira yasiyoridhisha kiafya.

11 Afisa Afya akigundua kuwa kuna mazingira yasiyoridhisha kiafya atatoa taarifa ya maandishi ya siku kumi na nne (14) kwa mhusika au Taasisi kumtaka arekebishe mazingira yake ndani ya muda huo.

Makosa

12 Itakuwa ni kosa chini ya Sheria Ndogo hizi kwa mtu yeyote:

a) Kujenga choo umbali wa mita 30 kutoka kisimani, ziwani, mtoni au chanzo kingine cha maji yanayotumika kwa matumizi ya binadamu;
b) Kutoa kinyesi au kusababisha kinyesi, mkojo, maji machafu yenye kinyesi kutoka kwenye choo chake au bafu lake au karo la kuoshea vyombo au nguo au kutoka kwenye bomba lolote linalochukua maji machafu na kuyatiririsha kwenye barabara, mitaa au kwenye mifereji ya maji ya mvua au mfereji wowote ulio wazi.
c) Kutupa takataka au kusababisha mtu mwingine atupe takataka au kusababisha mlundikano wa takataka mahali popote palipokataliwa na Halmashauri;
d) Kutiririsha maji machafu yanayoweza kusababisha kero kwa wakazi wa maeneo husika;
e) Kuuza chakula nje ya maeneo yaliyotengwa kwa ajili hiyo.

Adhabu

13 Mtu yeyote atakayevunja au kushindwa kutimiza masharti ya Sheria Ndogo hizi atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini ya shilingi elfu hamsini tu (50,000/=) au kifungo kisichozidi miezi kumi na mbili jela au adhabu zote mbili yaani faini na kifungo.

JEDWALI A: ADA ZA KUZOLEA TAKATAKA.

Sheria Ndogo 6(2)

Na	**Aina ya Biashara.**	**Ada kwa Mwezi(Tshs.)**
1	Baa na Maduka ya vinywaji (Groceries)	2,500/=
2	Migahawa na Mama Lishe	1,000/=
3	Nyumba za wageni	3,000/=
4	Kumbi za starehe na saluni	2,000/=
5	Majengo mengine ya biashara.	1,500/=
6	Nyumba za kuishi(makazi)	500/=
7	Vibanda au meza za biashara	1,000/=
8	Viwanda, fundi seremala na gereji	3,000/=
9	Wachoma chips, kuku, nyama n.k	1,500/=
10	Wauza mbao	2,000/=
11	Vioski	1,000/=
12	Maduka	3,000/=
13	Hotel	3,000/=
14	Bucha	3,000/=
15	Sheli ya mafuta	3,000/=
16	Mashine ya kusaga nafaka	2,000/=

JEDWALI B: ADA ZA UKAGUZI WA MAZINGIRA YA BIASHARA.

Sheria Ndogo 6(2)

Na	**Aina ya Biashara.**	**Ada kwa Mwaka (Tshs.)**
1	Baa na Maduka ya vinywaji (Groceries)	20,000/=
2	Migahawa na Mama Lishe	10,000/=
3	Nyumba za wageni	25,000/=
4	Kumbi za starehe na saluni	20,000/=
5	Majengo mengine ya biashara.	15,000/=
6	Vibanda au meza za biashara	5,000/=
7	Mafundi seremala na gereji	20,000/=
8	Wachoma chips, kuku, nyama	10,000/=
9	Wauza mbao	20,000/=
10	Saluni	12,000/=
11	Vioski	15,000/=
12	Maduka ya dawa za binadamu	20,000/=
13	Viwanda	100,000/=
14	Bucha	25,000/=
15	Maduka mbalimbali	25,000/=
16	Shelly	50,000/=
17	Mashine za kusaga nafaka	20,000/=
18	Hoteli za kitalii na za kawaida	100,000/=
19	Migodi ya madini	500,000/=
20	Zahanati/Hospitali binafsi	150,000/=
21	Shule binafsi	150,000/=
22	Vyuo binafsi	200,000/=

Lakiri ya Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa imewekwa kwenye Sheria Ndogo hizi kufuatia Azimio la Mkutano wa Baraza la Madiwani uliofanyika katika Ukumbi wa Halmashauri tarehe 11 mwezi Februari mwaka 2014 na kubandikwa mbele ya:-

……
William N. Waziri
Mkurugenzi Mtendaji (W)
Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa.

…….
Mathei Felician Kongo
Mwenyekiti wa Halmashauri.
Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa.

NAKUBALI,

……..……
MHE. MIZENGO .P. PINDA (MB)
WAZIRI MKUU

DODOMA,

TAREHE……